


# SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



## Kipimo Cha Wino Kuvuja



Ni picha nzuri ya kupendeza yenye nyota toka angani, iliyopigwa katika kituo cha kuangalia anga cha Ulaya ya Kusini! Lakini inaonekana kama kuna mtu amemwaga kitu katikati ya picha. Hivyo ndivyo mwanaanga wa kwanza aliyegeundua doa la angani alivyofikiria. Ingawa maneno yake halisia yalikuwa kimashairi zaidi: alilifanua kwa kusema "ni tone la wino katika anga ing'aayo".

Tunachokiangalia katika picha hii ni mamilioni ya nyota zinazong'aa kutoka katika sehemu ya galaxi yetu ya Milky Way ing'aayo sana. Katika sehemu ya anga iliyojaa nyota katika picha ni vigumu sana kuona sehemu ilio nyeusi. Ingawa katikati ya picha hiyo hiyo, karibu kabisa na nyota ing'aayo sana unaweza kuona wingu jeusi ambalo si la kawaida.

Unaweza kuona kama shimo lililowazi linaloikinga nyota, lakini shimo hili jeusi ni wingu dogo la vumbi lililojitenza mbele ya wigo wa nyota. Mawingu kama haya yanaitwa 'Bok globules'. Yametengenezwa na chembe chembe ndogo za vumbi ambazo zinakinga miale ya nyota inayotoka nyuma yake na kufanya eneo hilo lioneokane kama doa jeusi.

Bok globues ni masalia ya wingu kubwa linajulikanalo kama 'molecular clouds' au kwa jina rahisi ni 'stellar nurseries', kwa sababu nyota huzaliiwa katika mawingu hayo makubwa! Karibu nyota milioni kumi zenyenye ukubwa sawa na Jua zinazaliwa katika wingu moja la molecular cloud! Nyota katika kundi linalowaka lililopo pichani zimetengenezwa kutoka katika wingu moja la molecular clouds, na Bok globule iliyopo karibu yake ni sehemu ndogo iliyobakia.

### COOL FACT

Baadhi ya madaktari wa akili huwapa wagonjwa wao mtihani wa kuvuja kwa wino katika karatasi ili kuangalia afya ya akili. Kutokana na umbo la wino uliovuja lililotengenezwa katika karatasi daktari huweza kugundua tabia za mgonjwa anapoliangalia. Je unaona nini kwenye doa jeusi? Naona mjesi. Je unafikiri hilo jibu lina maana kwetu!



More information about EU-UNAWE  
Space Scoop: [www.eu-unawe.org/kids/](http://www.eu-unawe.org/kids/)